# 2 Petro

*Salamu*
1 Simoni Petro, mtumishi na mtume wa Isa Al-Masihi.

Kwa wale ambao kupitia kwa haki ya Mungu na Mwokozi wetu Isa Al-Masihi mmepokea imani iliyo na thamani kama yetu.

2 Neema na amani ziwe kwenu kwa wingi katika kumjua Mungu na Isa Bwana wetu.

*Wito wa Mfuasi wa Al-Masihi na uteule*
3 Uweza wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.
4 Kwa sababu hiyo, ametukirimia ahadi zake kuu na za thamani kupitia mambo haya, ili kupitia hayo mpate kuwa washiriki wa asili ya uungu, na kuokoka kutoka upotovu ulioko duniani unaosababishwa na tamaa mbaya.
5 Kwa sababu hii hasa, jitahidini sana katika imani yenu kuongeza wema; na katika wema, maarifa;
6 katika maarifa, kiasi; katika kiasi, saburi; katika saburi, utauwa;
7 katika utauwa, upendano wa kindugu; na katika upendano wa kindugu, upendo.
8 Kwa maana haya yakiwa ndani yenu kwa wingi na kuzidi kuongezeka, yatawasaidia kutokosa bidii wala kutokuzaa matunda katika kumjua Bwana wetu Isa Al-Masihi.

9 Lakini mtu yeyote asipokuwa na mambo
haya, haoni mbali na ni kipofu, naye amesahau
kwamba ametakaswa kutoka dhambi zake za
zamani.
10 Kwa hiyo, ndugu zangu, fanyeni bidii zaidi
kuuthibitisha wito wenu na uteule wenu. Kwa
maana mkifanya hivyo, hamtajikwaa kamwe,
11 na mtajaliwa kwa ukarimu mwingi kuingia
katika ufalme wa milele wa Bwana na Mwokozi
wetu Isa Al-Masihi.

*Unabii wa Maandiko*

12 Hivyo nitawakumbusha mambo haya siku
zote, hata ingawa mnayajua na mmethibitishwa
katika kweli mliyo nayo.
13 Naona ni vyema kuwakumbusha mambo
haya wakati wote niko katika hema hili ambalo
ni mwili wangu,
14 kwa sababu najua kwamba hivi karibuni
nitaliweka kando, kama vile Bwana wetu Isa Al-
Masihi alivyoliweka wazi kwangu.
15 Nami nitafanya kila juhudi kuona kwamba
baada ya kuondoka kwangu mtaweza kuyakum-
buka mambo haya siku zote.
16 Tulipowafahamisha kuhusu uweza na kuja
kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi, hatukufuata ha-
dithi zilizotungwa kwa werevu, bali tulishuhudia
kwa macho yetu ukuu wake.
17 Alipewa heshima na utukufu kutoka kwa
Mungu Baba* Mwenyezi, sauti ilipomjia katika

* **1:17** Jina Baba linaonesha uhusiano maalum wa Isa na Mwenyezi Mungu. Kwa mwanadamu, Mwenyezi Mungu ni Baba kupitia uhusiano unaopatikana katika kumtumaini Isa Al-Masihi.

Utukufu Mkuu, ikisema, “Huyu ni Mwanangu
mpendwa. Ninapendezwa naye sana.”
18 Sisi wenyewe tuliisikia sauti hii ambayo ili-
toka mbinguni, wakati tulipokuwa pamoja naye
kwenye ule mlima mtakatifu.
19 Nasi tunalo pia neno la hakika zaidi la un-
abii, ambalo mtafanya vyema mkiliangalia kwa
bidii, kama nuru inavyong’aa gizani, hadi ku-
pambazuke na nyota ya asubuhi izuke mioyoni
mwenu.
20 Zaidi ya yote, yawapasa mjue kwamba
hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa
kama alivyopenda nabii mwenyewe.
21 Kwa maana unabii haukuja kamwe kwa
mapenzi ya mwanadamu, bali watu walinena
yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho
Mtakatifu wa Mungu.

# 2

### *Walimu wa uongo na uangamizi wao*

1 Lakini pia waliinuka manabii wa uongo
miongoni mwa watu, kama watakavyokuwako
walimu wa uongo miongoni mwenu. Watain-
giza mafundisho yasiyopatana na kweli kwa siri,
hata kumkana Bwana Mungu Mwenyezi wa pe-
kee aliyewanunua, na hivyo kujiletea wenyewe
maangamizi ya haraka.
2 Nao wengi watafuata njia zao potovu, na kwa
ajili yao njia ya kweli itatukanwa.
3 Nao katika tamaa zao mbaya, walimu hawa
watajipatia faida kwenu kwa hadithi walizo-
tunga wenyewe. Lakini hukumu imekwisha

kutangazwa dhidi yao tangu zamani, wala uangamivu wao haujalala usingizi.

4 Kwa maana, kama Mungu hakuwasamehe malaika walipotenda dhambi, bali aliwatupa Kuzimu* katika vifungo vya giza wakae humo hadi ije hukumu;

5 kama hakuusamehe ulimwengu wa kale alipoleta gharika juu ya watu wale wasiomcha Mungu, lakini akamhifadhi Nuhu, mhubiri wa haki, pamoja na watu wengine saba;

6 kama aliihukumu miji ya Sodoma na Gomora kwa kuiteketeza kwa moto ikawa majivu, na kuifanya kuwa kielelezo kwa yale yatakayowapata wale wasiomcha Mungu;

7 na kama alimwokoa Lutu, mtu mwenye haki, ambaye alihuzunishwa na maisha machafu ya watu wapotovu

8 (kwa sababu yale matendo mapotovu aliyoyaona na kuyasikia huyo mtu mwenye haki alipoishi miongoni mwao yalimhuzunisha siku baada ya siku):

9 ikiwa hivyo ndivyo, basi Mwenyezi Mungu anajua jinsi ya kuwaokoa wamchao Mungu kutoka majaribu, na kuwaweka waasi katika adhabu hadi siku ya hukumu.

10 Hii ni hakika hasa kwa wale wanaofuata tamaa mbaya za mwili na kudharau mamlaka.

Kwa ushupavu na kwa kiburi, watu hawa hawaogopi kunena mabaya dhidi ya viumbe vya mbinguni.

---

* **2:4** Kuzimu hapa linalotokana na neno *Tartarus* la Kiyunani; maana yake ni kule ndani sana katika mahali pa mateso kwa watu waliopotea.

11 Lakini hata malaika, ijapokuwa wana nguvu
na uwezo zaidi, hawaleti mashtaka mabaya dhidi
ya viumbe kama hao mbele za Mwenyezi Mungu.
12 Lakini watu hawa hukufuru katika mambo
wasiyoyafahamu. Wao ni kama wanyama wasio
na akili, viumbe wanaotawaliwa na hisia za
mwili, waliozaliwa ili wakamatwe na kuchinjwa.
Hawa nao kama wanyama wataangamizwa pia.

13 Watalipwa madhara kwa ajili ya madhara
waliyowatendea wengine. Huhesabu kuwa ni
fahari kufanya karamu za ulevi na ulafi mchana
peupe. Wao ni mawaa na dosari, wakijifurahisha
katika anasa zao wanaposhiriki karamu pamoja
nanyi.
14 Wakiwa na macho yaliyojaa uzinzi, kamwe
hawaachi kutenda dhambi. Huwashawishi wale
wasio imara. Wao ni hodari kwa kutamani; ni
wana wa laana!
15 Wameiacha njia iliyo nyoofu, wakapotoka
na kuifuata njia ya Balaamu mwana wa Beori
aliyependa mshahara wa uovu.
16 Lakini kwa ajili ya uovu wake, alikemewa
na punda, mnyama asiyejua kusema, alipoongea
kwa sauti ya mwanadamu na kuzuia wazimu wa
huyo nabii.

17 Watu hawa ni chemchemi zisizo na maji, na
ukungu unaopeperushwa na tufani. Giza nene
limewekwa tayari kwa ajili yao.
18 Kwa maana wao hunena maneno matupu ya
kiburi. Nao wanavutia tamaa mbaya za asili ya
mwili, ili kuwashawishi watu ambao wanajion-
doa kutoka kwa wale wanaoishi katika hatia.

19 Wanawaahidi uhuru wakati wao wenyewe
ni watumwa wa upotovu; kwa maana “mtu ni
mtumwa wa chochote kinachomtawala.”
20 Kama wameukimbia upotovu wa dunia kwa
kumjua Bwana wetu na Mwokozi Isa Al-Masihi,
kisha wakanaswa tena humo na kushindwa, hali
yao ya mwisho ni mbaya kuliko ile ya kwanza.
21 Ingekuwa afadhali kwao kama hawangeijua
kamwe njia ya haki, kuliko kuijua kisha waka-
iacha ile amri takatifu waliyokabidhiwa.
22 Kwao mithali zimetukia kuwa za kweli,
zinaposema: “Mbwa huyarudia matapiko yake
mwenyewe,” tena, “Nguruwe aliyeoshwa hurudi
kugaagaa matopeni.”

# 3

*Siku ya Mwenyezi Mungu*

1 Wapendwa, huu ndio waraka wangu wa pili
ninaowaandikia. Katika nyaraka hizi mbili ni-
najaribu kuziamsha nia zenu safi kwa mawazo
makamilifu.
2 Nataka ninyi mkumbuke maneno
yaliyosemwa zamani na manabii watakatifu na
ile amri ya Bwana na Mwokozi wetu mliyopewa
kupitia kwa mitume wenu.
3 Kwanza kabisa, ni lazima mfahamu kwamba
siku za mwisho watakuja watu wenye dhihaka,
wakidhihaki na kuzifuata tamaa zao mbovu.
4 Watasema, “Iko wapi ile ahadi ya kuja kwake?
Tangu baba zetu walipofariki, kila kitu kinaen-
delea kama kilivyokuwa tangu mwanzo wa ku-
umbwa.”

5 Lakini wao kwa makusudi hupuuza ukweli
huu, kwamba kwa neno la Mungu mbingu zi-
likuwa tangu zamani, nayo dunia ilifanyizwa
kutoka ndani ya maji na kwa maji.
6 Ulimwengu wa wakati ule uligharikishwa
kwa hayo maji na kuangamizwa.
7 Kwa neno lilo hilo, mbingu za sasa na
dunia zimewekwa akiba kwa ajili ya moto,
zikihifadhiwa hadi siku ile ya hukumu na ya
kuangamizwa kwa watu wasiomcha Mungu.

8 Lakini wapendwa, msisahau neno hili:
kwamba kwa Mwenyezi Mungu, siku moja ni
kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku
moja.
9 Mwenyezi Mungu hakawii kuitimiza ahadi
yake, kama watu wengine wanavyokudhani
kukawia. Badala yake, yeye anawavumilia ninyi,
maana hataki mtu yeyote aangamie, bali kila mtu
afikilie toba.
10 Lakini siku ya Mwenyezi Mungu itakuja
kama mwizi. Ndipo mbingu zitatoweka
kwa kishindo kikuu; navyo vitu vya asili
vitateketezwa kwa moto, nayo dunia na kila
kitu kilicho ndani yake kitaunguzwa.

11 Kwa kuwa vitu vyote vitaharibiwa namna
hii, je, ninyi imewapasa kuwa watu wa namna
gani? Inawapasa kuishi maisha matakatifu na ya
kumcha Mungu,
12 mkingojea na kuhimiza kuja kwa hiyo siku
ya Mungu. Siku hiyo italeta mbingu kuchomwa
moto na kutoweka, na vitu vya asili vitayeyuka
kwa moto.

13 Lakini kufuatana na ahadi yake, sisi tu-
natazamia mbingu mpya na dunia mpya, ambayo
haki hukaa ndani yake.
14 Kwa sababu hii, wapendwa, kwa kuwa
mnatazamia mambo haya, fanyeni bidii ili
awakute bila mawaa wala dosari, na mkiwa na
amani kwake.
15 Hesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa
ni wokovu, kama vile ndugu yetu mpendwa
Paulo alivyowaandikia kwa hekima ile aliyopewa
na Mungu.
16 Huandika vivyo hivyo katika nyaraka zake
zote, akizungumzia ndani yake mambo haya.
Katika nyaraka zake kuna mambo mengine
ambayo ni vigumu kuyaelewa, ambayo watu
wajinga na wasio thabiti huyapotosha, kama
wanavyopotosha Maandiko mengine na kujiletea
maangamizi yao wenyewe.
17 Basi, ninyi wapendwa, kwa kuwa
mmekwisha kujua mambo haya, jilindeni msije
mkachukuliwa na kosa la watu hao waasi na
kuanguka kutoka kwa uthabiti wenu.
18 Bali kueni katika neema na katika kumjua
Bwana na Mwokozi wetu Isa Al-Masihi.

Utukufu una yeye sasa na milele! Amen.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible." Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d